**SHERIA YA KUANZISHA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**MPANGILIO WA VIFUNGU**


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA KWA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR**

4. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.
5. Muhuri na nembo ya Mfuko.
6. Malengo ya Mfuko.
7. Kazi za Mfuko.

**SEHEMU YA TATU**
**UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA MFUKO**

8. Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.
9. Sifa za Mwenyekiti.
10. Katibu wa Bodi.
11. Kazi za Bodi.
12. Uwezo wa Bodi.
13. Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

14. Posho la wajumbe.

15. Mwenendo wa Bodi.

16. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

17. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

18. Idara, Divisheni na Vitengo vya Mfuko.

19. Wafanyakazi wa Mfuko.

**SEHEMU YA NNE**
**USAJILI WA MWANACHAMA NA UKUSANYAJI WA MICHANGO**

20. Usajili wa mwanachama.

21. Kitambulisho cha Uanachama.

22. Michango na viwango vya michango.

**SEHEMU YA TANO**
**HUDUMA ZA AFYA**

23. Kitita cha Huduma.

24. Haki za mwanachama.

25. Muda wa kusubiri.

26. Stahiki za huduma za afya kwa Wastaafu.

27. Huduma za afya nje ya Zanzibar.

**SEHEMU YA SITA**
**WATOA HUDUMA ZA AFYA**

28. Uthibitisho wa watoa huduma za afya.

29. Mfumo wa malipo.

30. Uwasilishaji wa madai ya malipo.

31. Uhakiki wa ubora.

32. Mfumo wa tathmini.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA


33. Vyanzo vya Fedha.

34. Matumizi ya fedha za Mfuko.

35. Fedha za Mfuko kuwa chini ya dhamana ya Bodi.

36. Usimamizi wa fedha za Mfuko.

37. Bajeti ya Mfuko.

38. Taarifa ya ukaguzi wa Mfuko.

39. Uwezo wa kukopa.

40. Uanzishwaji wa Akaunti ya Hesabu ya Usawa.


## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU


41. Makosa na Adhabu.

42. Adhabu kwa kushindwa kusajili.

43. Adhabu ya jumla.


## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO


44. Tathmini ya Uhimilivu wa Mfuko.

45. Ulazima wa kuwa na bima ya afya.

46. Uhamishaji wa bima ya afya.

47. Hifadhi ya michango.

48. Taarifa ya mwaka.

49. Msamaha wa kodi.

50. Marekebisho yenye athari.

51. Matumizi ya Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

52. Kanuni.


## JADWELI

**SHERIA NAM. 1 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

20 Machi, **2023**

# SHERIA YA KUANZISHA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar, 2023 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti.

Matumizi.

**2.**-(1) Sheria hii itatumika kwa:

(a) wafanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi;

(b) wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi;

(c) wageni wanaoishi Zanzibar ambao ukaazi wao unazidi miezi sita;

(d) wastaafu;

(e) wanafunzi wanaosoma vyuo au taasisi za elimu ya juu Zanzibar isipokuwa wale watakaokuwa wategemezi wa Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii; na

(f) wakaazi wote wa Zanzibar.

(2) Utekelezaji wa Sheria hii utaanza kwa kundi lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki, ambao watajisajili na kuwa wanachama wa Mfuko mara baada ya Sheria hii kuanza kutumika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utekelezaji kwa makundi yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) (b), (c), (d), (e) na (f) utafanyika kama itakavyoainishwa na Waziri kupitia tangazo litakalochapishwa katika Gazeti.

(4) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Bodi na kwa tangazo lilochapishwa katika Gazeti, kuingiza au kutoa kundi lolote kuwa mwanachama wa Mfuko kama atakavyoona inafaa.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Uthibitisho" maana yake ni hatua ya kuwathibitisha watoa huduma za afya ili waweze kutoa huduma za afya;

"Mtathmini" maana yake ni mtaalamu yeyote mwenye sifa ya kufanya tathmini ya uhimilivu wa Mfuko;

"Kitita cha huduma" maana yake ni huduma za afya zinazotolewa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Uhusiano wa damu" maana yake ni uhusiano wa ndugu wa karibu unaotokana na kuzaliwa au kizazi;

"Mtoto" maana yake ni mtu ambaye yupo chini ya umri wa miaka kumi na nane au chini ya umri wa miaka ishirini na moja ikiwa anaendelea na masomo ambaye hajaoa au kuolewa na asiye na ajira;

"Mchango" maana yake ni kiwango kinacholipwa na mwanachama au mwajiri katika Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mtegemezi" maana yake:

(a) mtoto wa kuzaa mwenyewe;

(b) mtoto wa kuasili au kulea ambae mahitaji yake ya lazima yapo chini ya usimamizi wa mwanachama;

(c) Mwenza na mzazi ambae hayupo katika sekta rasmi au isiyo rasmi na hana kipato cha kuchangia.

"Muajiriwa" maana yake ni mtu yeyote ambaye ameajiriwa kwa mkataba na ambaye anapokea au anastahiki kupokea mshahara;

"Muajiri" maana yake ni mtu yeyote ambaye ameingia mkataba wa ajira na muajiriwa kwa malipo ya mshahara;

Sekta rasmi" maana yake ni sekta inayojumuisha kazi zote zinazofanywa kwa mujibu wa saa za kazi kisheria na mshahara unatambulika kama chanzo cha mapato ambacho kodi ya mapato inalipwa;

"Mgeni" maana yake ni mtu yeyote anayeingia Zanzibar kutoka sehemu yoyote nje ya Zanzibar kwa lengo la kutembea, kutalii, biashara na anabakia Zanzibar kwa muda maalum;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar ulioanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Mtoa Huduma za Afya" maana yake ni taasisi yoyote ya afya iliyopewa leseni ya kutoa huduma za afya na kuthibitishwa na Mfuko;

"Sekta isiyo rasmi" maana yake ni sekta ambayo inajumuisha wafanyakazi waliojiajiri wenyewe, au wanaofanyakazi kwa watu waliojiajiri wenyewe ambao hawamo katika mfumo maalumu wa mishahara na hawana muda maalumu wa kufanya kazi;

"Huduma za kulazwa" maana yake ni huduma za afya zinazohusiana na kulazwa kwa mgonjwa hospitalini au kituo chengine chochote cha afya kwa ajili ya matibabu kwa angalau siku moja au zaidi;

"mwanachama" maana yake ni mtu yeyote ambaye amesajiliwa katika Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Kitambulisho cha Uanachama" maana yake ni kadi maalum ya uanachama wa Mfuko kilichotolewa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na Mfuko;

"Wizara" maana yake ni Wizara inayohusika na Afya;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Uhakiki wa Ubora wa Huduma" maana yake ni mapitio na tathmini ya ubora wa huduma zinazotolewa na watoa huduma;

"Wakaazi wa Zanzibar" maana yake ni watu wote wanaoishi Zanzibar bila ya kujali utaifa wao ambao wametimiza masharti ya ukaazi wa Zanzibar kwa mujibu wa sheria zinazohusika;

"Mstaafu" maana yake ni mwanachama wa Mfuko aliyestaafu kazi kwa mujibu wa sheria zinazohusika;

"Mshahara" maana yake ni mshahara jumuishi unaotokana na mkataba wa ajira; na

"Makundi maalumu" inajumuisha watu wasio na uwezo, watoto yatima, wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, Watu Wenye Ulemavu wasiokuwa na uwezo na kundi jengine lolote litakalotangazwa na Waziri.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.

(2) Mfuko utakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri wake na kupitia jina lake kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba, ubia au miamala ya kibiashara kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(d) kukopa fedha kutoka katika taasisi yoyote ya kifedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(e) kutekeleza au kufanya jambo lolote ambalo kisheria linaweza kufanywa au kutekelezwa na chombo kinachojitegemea.

Muhuri na nembo ya Mfuko.

**5.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Mfuko katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Mfuko katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Mkurugenzi Mkuu au Afisa mwengine yeyote wa Mfuko atakayeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Mfuko utawekwa muhuri wa Mfuko na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Mfuko.

**6.** Malengo ya Mfuko yatakuwa ni:

(a) kufikia upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote, za uhakika na endelevu kwa wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar; na

(b) upatikanaji wa rasilimali fedha za kutosha na endelevu za kugharamia huduma za afya kwa wote.

Kazi za Mfuko.

**7.** Mfuko utakuwa na kazi ya:

(a) kusajili wanachama wa Mfuko na watoa huduma;

(b) kukusanya, kuhifadhi na kusimamia michango na fedha nyengine zitakazolipwa katika Mfuko kwa kufuata masharti yaliyowekwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

(c) kulipia huduma za afya kwa wanachama na wategemezi wao;

(d) kulinda maslahi ya wanachama;

(e) kufanya ukaguzi kwa watoa huduma za afya na wanaoomba kuthibitishwa kutoa huduma za afya;

(f) kuweka na kuhifadhi kumbukumbu au taarifa za kila mwanachama zinazohusu malipo ya michango na huduma zilizotolewa na Mfuko;

(g) kuandaa miongozo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Mfuko;

(h) kuwekeza ziada ya fedha za Mfuko zilizokusanywa kutoka vyanzo mbali mbali katika miamala halali ya kibiashara na kwa mujibu wa miongozo ya uwekezaji ya Mfuko kama Bodi itakavyoona inafaa;

(i) kupokea huduma kutoka kwa mtu au taasisi yoyote ya umma au binafsi kwa ajili ya kutekeleza kazi maalum za Mfuko;

(j) kuhakikisha hesabu za Mfuko zinafungwa na zinakaguliwa kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya sheria zinazohusika;

(k) kufanya au kuwezesha kufanyika tathmini ya uhimilivu wa Mfuko na tafiti mbali mbali juu ya hali ya fedha za Mfuko kila baada ya kipindi cha miaka mitatu; na

(l) kufanya jambo lolote ambalo linaweza kupelekea utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA MFUKO

Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.

**8.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mjumbe mmoja kutoka:

(i) Wizara inayohusika na Afya;

(ii) Wizara inayohusika na Fedha;

(iii) Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar;

(iv) Jumuiya ya Waajiri Zanzibar; na

(v) Jumuiya ya Watoa Huduma za Afya kutoka sekta binafsi.

(2) Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(c) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia jinsia ikiwa watu hao:

(a) wana angalau shahada ya kwanza katika fani ya afya, afya ya jamii, uchumi, bima, fedha, biashara au fani nyengine yoyote inayolingana nazo kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) wana uzoefu wa kazi wa angalau miaka mitano na

(c) wana uadilifu wa hali ya juu.

Sifa za Mwenyekiti.

**9.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya afya, afya ya jamii, uchumi, bima, fedha, utawala, biashara, hifadhi ya jamii, sheria au fani nyengine yoyote inayolingana nazo kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**10.**-(1) Bodi itamteua mtumishi wa Mfuko mwenye sifa kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria; au mtu mwenye sifa za kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na atakuwa na kazi ya:

(a) kuandaa ajenda pamoja na kuchukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(b) kutunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) kutoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(d) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria.

Kazi za Bodi.

**11.** Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kusimamia uendeshaji wa jumla wa Mfuko;

(b) kupitia na kuidhinisha miongozo, mipango na bajeti ya Mfuko;

(c) kuhakikisha Mfuko unalipa fedha za huduma zilizotolewa na watoa huduma kwa wakati;

(d) kuidhinisha kitita cha huduma;

(e) kutoa miongozo juu ya utekelezaji wa mpango mkakati na bajeti ya Mfuko ya kila mwaka;

(f) kutoa na kusimamia miongozo ya ndani ya watumishi;

(g) kumshauri Waziri juu ya mambo yote yanayohusiana na uimarishaji na uendelezaji wa Mfuko;

(h) kuwathibitisha watoa huduma za afya;

(i) kuhakikisha makusanyo na madeni ikijumuisha michango isiyolipwa inapatiwa ufumbuzi ipasavyo;

(j) kuwasilisha kwa Waziri taarifa ya robo mwaka na ya mwaka ambayo itajumuisha taarifa kuhusu hali ya Mfuko; na

(k) kufanya kazi nyengine yoyote itakayokuwa muhimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

**12.** Bodi itakuwa na uwezo wa:

(a) kuanzisha kamati za Bodi na kukasimu sehemu ya mamlaka yake kwa kamati hizo au kwa mfanyakazi yeyote wa Mfuko, endapo itahitajika;

(b) kuajiri wafanyakazi wa Mfuko;

(c) kuweka viwango vya huduma zinazotolewa.

(d) kuandaa kanuni za utumishi na kanuni za fedha;

(e) kuanzisha matawi ya ofisi ya Mfuko endapo itaonekana inafaa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(f) kusimamia masuala ya kinidhamu kwa watumishi wa Mfuko kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

**13.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Posho la wajumbe.

**14.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine zinazohusika.

Mwenendo wa Bodi.

**15.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yataainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**16.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya afya ya jamii, afya, bima, uchumi, fedha, biashara, hifadhi ya jamii, sheria au fani nyengine yoyote inayolingana nazo kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**17.**-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko na atatekeleza kazi za kila siku za Mfuko na atawajibika kwa Bodi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu:

(a) atasimamia utekelezaji wa malengo ya Mfuko;

(b) atakusanya na kusimamia michango, fedha, rasilimali na malipo mengine ya Mfuko;

(c) atawajibika kwa mapato na matumizi yote ya Mfuko;

(d) atafanya majadiliano na kuingia mikataba na watoa huduma wa afya baada ya kuidhinishwa na Bodi;

(e) ataanzisha na kutunza daftari la kumbukumbu la wanachama, watoa huduma wa afya na waajiri;

(f) atalinda na kuendeleza maslahi ya wanachama kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(g) ataandaa mipango ya muda mfupi na mrefu na bajeti ya mwaka;

(h) atachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wa Mfuko baada ya kuidhinishwa na Bodi na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(i) atawasilisha taarifa za kazi na fedha za Mfuko kwa Bodi; na

(j) atafanya kazi zote atakazoelekezwa na Bodi kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Idara, divisheni na vitengo vya Mfuko.

**18.**-(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa kazi za Mfuko, Bodi inaweza kuanzisha idara, divisheni au vitengo kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakuu wa idara watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni na vitengo watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, divisheni na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi wa Mfuko.

**19.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Bodi itaajiri wafanyakazi kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Mfuko.

## SEHEMU YA NNE
## USAJILI WA WANACHAMA NA UKUSANYAJI WA MICHANGO

Usajili wa wanachama.

**20.**-(1) Watu wote walioainishwa katika kifungu cha 2(1) cha Sheria hii, watajisajili kuwa wanachama wa Mfuko kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

(2) Kila mwajiri atawasilisha, ndani ya siku tisini baada ya kuanza kutumika Sheria hii au ndani ya siku thelathini tokea tarehe ya kumwajiri mfanyakazi husika, orodha ya wafanyakazi wake kwa Mfuko kwa ajili ya usajili.

Kitambulisho cha Uanachama.

**21.**-(1) Kutakuwa na Kitambulisho cha Uanachama kitakachotolewa na Mfuko kwa mwanachama baada ya kutimiza masharti ya usajili.

(2) Kitambulisho cha Uanachama kitatumika kwa ajili ya utambulisho na uthibitisho wa mwanachama wakati anahitaji huduma za afya.

Michango na viwango vya michango.

**22.**-(1) Kila mwanachama atachangia katika Mfuko kiwango maalum cha michango kilichoainishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

(2) Viwango vya michango kwa wanachama kutoka sekta isiyo rasmi vitaainishwa na kutangazwa na Waziri kwa kushauriana na Bodi na kwa kuzingatia makundi ya wanachama yaliyoainishwa katika Sheria hii.

(3) Michango ya wanachama kutoka sekta ya umma na binafsi itawasilishwa na mwajiri katika Mfuko ndani ya siku kumi na nne baada ya siku ya mwisho wa mwezi husika.

(4) Mwajiri yeyote ambaye atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

(5) Mahakama itakayomtia hatiani, pamoja na adhabu iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, itamtaka mtu huyo kulipa deni la michango yote ambayo mwajiri huyo hajalipa.

## SEHEMU YA TANO
## HUDUMA ZA AFYA

Kitita cha Huduma.

**23.**-(1) Kutakuwa na kitita cha huduma ambacho kitatolewa kwa wanachama wa Mfuko pamoja na wategemezi wao.

(2) Kitita cha huduma kitajumuisha huduma zote muhimu za afya kama zilivyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Bodi na kwa kupitia tangazo litakalochapishwa katika Gazeti, kuongeza, kuondoa au kupunguza huduma yoyote ya afya zilizoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii endapo ataona inafaa kwa kuzingatia hali halisi ya kifedha ya Mfuko.

(4) Waziri baada ya kushauriana na Bodi atatoa miongozo itakayoainisha masharti ya utoaji wa kitita cha huduma zitakazotolewa kulingana na makundi ya wanachama yaliyoainishwa katika kifungu cha 2(1) cha Sheria hii.

Haki za wanachama.

**24.** Mwanachama atakuwa na haki ya kupata au kupatiwa huduma za afya na taarifa kupitia Mfuko kwa mujibu wa kitita cha huduma kilichoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii au miongozo itakayotolewa na Waziri.

Muda wa kusubiri.

**25.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 24 cha Sheria hii, kutakuwa na muda maalum wa kusubiri kuanza kupata huduma za afya kupitia Mfuko ambao utaainishwa katika Kanuni kwa kila kundi la wanachama lililoainishwa katika kifungu cha 2(1) cha Sheria hii.

Stahiki za huduma za afya kwa Wastaafu.

**26.**-(1) Mwanachama aliyestaafu kazi ambaye amechangia kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, atastahiki kupata huduma za afya yeye na wategemezi wake kwa kuchangia kiwango maalum kitakachoainishwa na Mfuko.

(2) Kiwango na utaratibu wa uchangiaji kwa mwanachama aliyestaafu katika sekta rasmi utaainishwa katika kanuni.

(3) Kiwango na utaratibu wa uchangiaji kwa mwanachama kutoka sekta isiyo rasmi aliyefikia umri wa miaka sitini utaainishwa katika kanuni.

Huduma za afya nje ya Zanzibar.

**27.**-(1) Mfuko utaandaa na kuweka utaratibu mahsusi na miongozo ambayo itawawezesha wanachama wake kupata huduma za afya nje ya Zanzibar kulingana na mahitaji ya huduma husika na hali halisi ya uwezo wa Mfuko.

(2) Utaratibu wa wanachama kupata huduma za afya nje ya Zanzibar utatangazwa na Waziri kupitia Gazeti au utaainishwa katika kanuni.

## SEHEMU YA SITA
## WATOA HUDUMA ZA AFYA

Uthibitisho wa watoa huduma za afya.

**28.**-(1) Kutakuwa na Watoa Huduma za Afya ambao watathibitishwa na Mfuko kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya kwa wanachama wa Mfuko.

(2) Mtoa Huduma za Afya anayetaka kutoa huduma za afya kwa wanachama atafanya maombi ya kuthibitishwa kwa Mkurugenzi Mkuu kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

(3) Utaratibu wa uombaji, utoaji, uhuishaji, usitishaji au ufutaji wa uthibitisho, urejeshaji, sababu za urejeshaji na ufutaji wa usajili na mambo mengine yanayohusiana na uthibitishaji yataainishwa katika kanuni.

Mfumo wa malipo.

**29.**-(1) Mtoa Huduma za Afya atalipwa na Mfuko baada ya kutoa huduma na kuwasilisha madai ya malipo kwa mujibu wa huduma alizotoa.

(2) Bodi inaweza kuweka mfumo mwengine wa malipo kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Mfuko.

(3) Fedha zote zitakazolipwa kwa Mtoa Huduma za Afya zitalipwa moja kwa moja katika hesabu ya benki ya mtoa huduma husika.

Uwasilishaji wa madai ya malipo.

**30.**-(1) Mtoa huduma yeyote atawasilisha maombi ya madai ya malipo katika Mfuko ndani ya siku thelathini baada ya kutoa huduma.

(2) Mfuko utafanya malipo ndani ya siku thelathini baada ya kupokea maombi ya malipo.

(3) Endapo Mfuko, ndani ya kipindi kilichotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, utashindwa kufanya malipo, utatoa taarifa kwa Mtoa Huduma za Afya anayehusika pamoja na sababu za kushindwa kufanya malipo hayo.

Uhakiki wa ubora.

**31.** Mfuko utafanya uhakiki wa ubora wa huduma, mapitio ya matumizi ya huduma na tathmini ya teknolojia inayotumika katika kutoa huduma kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa na Mfuko, kila baada ya muda, kwa lengo la kuhakikisha kwamba:

(a) huduma bora za matibabu zinatolewa kwa mujibu wa rasilimali zinazotumika, utaratibu unaotumika na matokeo yanayofikiwa yanakwenda sambamba na viwango vilivyowekwa na Mfuko kwa kuzingatia maadili ya afya;

(b) upatikanaji na utumiaji wa teknolojia na vifaa tiba vinakwenda sambamba na wakati, mahitaji halisi na viwango vinavyokubalika vya kitabibu; na

(c) utekelezaji wa taratibu za kitabibu, usimamizi na utoaji wa dawa unakwenda sambamba na viwango vinavyokubalika vya kitabibu na maadili yaliyowekwa na Wizara.

Mfumo wa tathmini.

**32.**-(1) Mfuko utaanzisha mfumo wa tathmini ambao utatekelezwa kupitia mkataba na watoa huduma na mfumo wa udhibiti ambao utahakikisha udhibiti dhidi ya:

(a) matumizi ya huduma yaliyopitiliza;

(b) vipimo visivyokuwa vya lazima vya uchunguzi na taratibu za kitabibu; na

(c) utaratibu wa rufaa za kitabibu usiofuata miongozo.

(2) Mfuko unaweza kukataa kulipa madai yote au kupunguza sehemu ya madai hayo iwapo mtoa huduma:

(a) amewasilisha madai yasiyo sahihi;

(b) amewasilisha taarifa zisizo sahihi; au

(c) ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii, kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii au miongozo iliyowekwa.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya Fedha.

**33.** Fedha na rasilimali za Mfuko zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zilizopokelewa na Mfuko kutokana na huduma zinazotolewa na Mfuko;

(c) ruzuku halali, zawadi, msaada, michango au mikopo kama Mfuko utakavyopokea kutoka kwa mtu yeyote au taasisi;

(d) mapato yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Mfuko; na

(e) fedha nyengine yoyote inayoweza kupatikana kihalali na Mfuko kutokana na utekelezaji wa kazi zake au vyenginevyo.

Matumizi ya fedha za Mfuko.

**34.-**(1) Matumizi ya fedha za Mfuko yatatumika kwa ajili ya kulipia madai kwa watoa huduma za afya, uendeshaji wa Mfuko na uwekezaji.

(2) Mfuko utawekeza ziada ya fedha itakayobaki katika namna ambayo itaidhinishwa na Bodi baada ya kuzingatia:

(a) kuwa na kiwango cha kutosha cha fedha za uendeshaji wa Mfuko;

(b) upatikanaji wa faida ya uwekezaji katika uwekezaji unaokusudiwa; na

(c) ushauri na maelekezo kutoka mamlaka zinazohusika.

Fedha za Mfuko kuwa chini ya dhamana ya Bodi.

**35.**-(1) Mfuko, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, utafungua hesabu ya benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi ulizopewa chini ya Sheria hii.

(2) Fedha zilizowekwa katika hesabu za benki za Mfuko ulioanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hazitokuwa au kuchukuliwa kuwa ni fedha za Mfuko lakini kwa madhumuni ya Sheria hii, zitachukuliwa kuwa ni fedha zilizo chini ya dhamana ya Bodi kama ni amana ya wanachama wa Mfuko.

(3) Mkurugenzi Mkuu atafanya malipo ya fedha kutoka katika hesabu za benki za Mfuko kwa kazi yoyote ambayo imeruhusiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Usimamizi wa fedha za Mfuko.

**36.** Matumizi, mpango wa uwekezaji, utoaji wa fedha, utawala na usimamizi wa Mfuko utaongozwa na Bodi kwa masharti kwamba:

(a) fedha za Mfuko zitatumika kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kanuni zake; na

(b) uwekezaji wowote wa Mfuko utakuwa na dhamana ya muda mfupi ambao utakuwa na faida, salama na halali kwa mujibu wa masharti ya sheria kama itakavyoelekezwa katika sera ya uwekezaji wa Mfuko.

Bajeti ya Mfuko.

**37.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, katika kila mwaka wa fedha, atawasilisha katika Bodi kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo juu ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi kwa ajili ya Mfuko kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na miongozo mengine yoyote inayoweza kutolewa na Serikali kila baada ya muda.

(3) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Mfuko ni sahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha unadumishwa juu ya mali na madeni ya Mfuko.

Taarifa ya ukaguzi wa Mfuko.

**38.** Mfuko utakaguliwa na kutolewa taarifa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Sheria ya Uanzishaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uwezo wa kukopa.

**39.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mfuko, kwa idhini ya Bodi, unaweza kukopa kiwango chochote cha fedha ambacho kitahitajika kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake.

(2) Ukopaji wa fedha utazingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na baada ya kupata idhini ya maandishi ya Waziri anayehusika na fedha.

(3) Mfuko hautoweka rehani mali zake kama ni dhamana ya mkopo wowote bila ya idhini ya maandishi ya Bodi.

Uanzishwaji wa Akaunti ya Hesabu ya Usawa.

**40.**-(1) Kutakuwa na Akaunti ya Hesabu ya Usawa ambayo itapokea na kuweka fedha inayotokana na kodi maalumu kutoka Serikalini, mashirika ya maendeleo, taasisi zisizo za kiserikali, kampuni au vyanzo vyengine halali.

(2) Fedha zilizowekwa katika Akaunti ya Hesabu ya Usawa zitatumika kugharamia utoaji wa huduma za afya kwa watu wasiokuwa na uwezo na makundi maalum.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na Adhabu.

**41.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anatoa taarifa au nyaraka zisizo sahihi kwa lengo la kukwepa kuchangia au kupata huduma asizostahili za Mfuko;

(b) anakataa au anashindwa kuwasilisha vielelezo au nyaraka zinazohitajika;

(c) anashindwa kulipa michango kwa mujibu wa masharti yaliowekwa chini ya Sheria hii au kanuni;

(d) anamzuia afisa wa Mfuko kutekeleza majukumu yake aliyopewa chini ya Sheria hii;

(e) anaghushi, anadanganya, anabadilisha au anakusudia kughushi kubadilisha au kudanganya kitambulisho cha mwanachama;

(f) anamkosesha mwanachama kupata huduma za afya kama anavyostahiki;

(g) anapokea faida yoyote ambayo hastahili chini ya Sheria hii;

(h) anakataa kujibu swali aliloulizwa au anajibu huku akijua kwamba majibu yake sio sahihi iwapo inaaminika kuwa ana taarifa hizo;

(i) anashindwa kuweka na kuwasilisha kumbukumbu sahihi zinazohusiana na huduma za afya; au

(j) anashirikiana na mtu yeyote kuvunja masharti ya Sheria hii,

ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

Adhabu kwa kushindwa kusajili.

**42.**-(1) Mtu yeyote ambaye anatakiwa kusajiliwa chini ya masharti ya Sheria hii na akashindwa kujisajili kuwa mwanachama wa Mfuko, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa kiwango cha michango kwa muda wote ambao ameshindwa kujisajili.

(2) Mwajiri yeyote ambaye atashindwa kuwasilisha taarifa za wafanyakazi wake katika Mfuko kwa ajili ya kusajiliwa chini ya masharti ya Sheria hii, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili.

(3) Pamoja na adhabu chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mwajiri atalipa kiwango cha michango kwa muda wote ambao alishindwa kuwasilisha taarifa za wafanyakazi wake katika Mfuko kwa ajili ya kusajiliwa na kulipa michango ya wafanyakazi wake.

Adhabu ya jumla

**43.** Mtu ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu chochote cha Sheria hii, kanuni, miongozo au amri yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii ambapo adhabu yake haikutajwa, ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Tathmini ya Uhimilivu wa Mfuko.

**44.**-(1) Mfuko utafanyiwa tathmini ya uhimilivu ambayo itafanywa na Mtathmini kwa kila miaka mitatu au kipindi chengine chochote ambacho Bodi itaona ni muhimu kufanya tathmini.

(2) Ripoti ya Tathmini ya Uhimilivu wa Mfuko itawasilishwa kwa Bodi na Waziri kwa ajili ya utekelezaji.

Ulazima wa kuwa na bima ya afya.

**45.**-(1) Mgeni yeyote anayetaka kuja Zanzibar anatakiwa awe na bima ya afya ambayo inatumika Zanzibar.

(2) Endapo mgeni atakuwa hana bima hiyo ya afya iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atalipia gharama za matibabu kwa Mtoa Huduma za Afya kwa gharama zake binafsi.

Uhamishaji wa bima ya afya.

**46.**-(1) Mfuko unaweza kuingia makubaliano na Mfuko mwengine wowote wa Bima ya Afya uliyopo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au katika nchi nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Bodi kila baada ya muda ili kuwawezesha wanachama wa Mfuko kupata huduma za afya.

(2) Katika utekelezaji wa makubaliano ambayo Mfuko umeingia, Bodi itahakikisha kuwa uhimilivu wa Mfuko na maslahi ya wanachama yanalindwa na kwa vyovyote kwamba hayaathiriwi na makubaliano hayo.

Hifadhi ya michango.

**47.** Fedha zinazolipwa na mwanachama zitakuwa ni mali ya Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na hazitokuwa sehemu ya mali ya mwanachama ikiwa atafilisika hazitatumika kulipia madeni.

Taarifa ya mwaka.

**48.** Bodi, ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kumalizika kwa kila mwaka wa fedha, itaandaa na kuwasilisha kwa Waziri taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya Mfuko ya mwaka husika

Msamaha wa kodi

**49.** Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote:

(a) kodi ya mapato haitolipwa kwa michango na mafao chini ya Sheria hii; na

(b) kodi ya ushuru wa stempu haitolipwa katika risiti au nyaraka yoyote iliyotolewa au iliyofanyiwa kazi na Bodi kwa niaba ya Mfuko au iliyotolewa na mtu mwengine yeyote anayehusiana na mafao au michango chini ya Sheria hii.

Marekebisho yenye athari.

**50.**-(1) Kifungu cha 27 cha Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja Nam. 3 ya 2016 kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 27 kama ifuatavyo:

"Huduma za afya.

**27.** Huduma za afya zitaendelea kutolewa na Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mujibu wa maelekezo ya Wizara na Sheria zinazotumika Zanzibar."

Matumizi ya Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

**51.**-(1) Katika kuhakikisha upatikanaji na utoaji wa huduma bora, Mfuko utaanzisha na kutumia mifumo ya kieletroniki mbali mbali na teknolojia ya habari na mawasiliano.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mfuko utalinda, utatunza na kuimarisha taarifa za wanachama katika hali ya usiri kwa wakati wote.

Kanuni.

**52.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

---

## MWENENDO WA BODI
**(Chini ya kifungu cha 15)**

---

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**1.** Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**2.**-(1) Bodi itakutana kila robo mwaka na inaweza kukutana katika vikao vya dharura muda wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**3.** Akidi katika vikao vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya idadi ya jumla ya wajumbe wake.

Maamuzi ya Bodi.

**4.** Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa makubaliano, ikiwa hakuna makubaliano, uamuzi utafanywa kwa wingi wa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Taratibu za vikao.

**5.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itaandaa taratibu zake zenyewe za vikao vyake.

Mjumbe mualikwa.

**6.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote mtaalamu kuhudhuria katika kikao cha Bodi, lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kubainisha maslahi.

**7.**-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni wa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya maamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**8.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) isipokuwa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu, ikiwa atasitishwa na Waziri endapo hatokidhi matarajio ya Mfuko;

(e) ikiwa mjumbe atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza; au

(f) kifo.

## JADWELI LA PILI

---

## MICHANGO NA VIWANGO VYA MICHANGO
**[Chini ya kifungu cha 22(1)]**

---

Kiwango cha michango kwa sekta ya umma na sekta binafsi.

**1.** Kiwango cha michango kitakachochangiwa katika Mfuko kwa wanachama kutoka sekta ya umma na sekta binafsi kitakuwa ni asilimia saba ya mshahara jumuishi wa mfanyakazi husika ambacho kitachangiwa kwa pamoja baina ya mwajiri na mwajiriwa.

Kiwango cha michango kwa Mwajiri.

**2.**-(1) Kila mwajiri wa sekta ya umma na binafsi atamchangia mfanyakazi wake katika Mfuko michango ya kila mwezi ya kiwango cha asilimia tatu na nusu ya mshahara jumuishi wa mwezi wa mfanyakazi husika.

(2) Kila mfanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi atachangia katika Mfuko asilimia tatu na nusu ya mshahara wake jumuishi wa mwezi kwa kila mwezi.

Kiwango cha michango kwa sekta isiyo rasmi.

**3.** Kiwango cha michango kwa wanachama kutoka sekta isiyo rasmi na makundi mengine ya wanachama kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 2 cha Sheria hii kitatangazwa na Waziri kupitia Gazeti Rasmi la Serikali baada ya Waziri kuingiza kundi husika kuwa mwanachama wa Mfuko au kutangaza Sheria hii kutumika kwa kundi husika.

## JADWELI LA TATU

## KITITA CHA HUDUMA ZA MFUKO
**[Chini ya kifungu cha 23(2)]**

1. Kitita cha huduma kwa wanachama wa Mfuko kitajumuisha:

(a) Huduma ya kumuona daktari;

(b) Huduma za wagonjwa wa nje na kulazwa;

(c) Vipimo vya maabara, mionzi na huduma nyengine za uchunguzi wa afya;

(d) Dawa na vifaa tiba na vifaa vyengine vya matibabu vilivyosajiliwa na vinavyoruhusiwa na Mamlaka husika kutumika Zanzibar;

(e) Huduma za upasuaji;

(f) Huduma za afya ya kinywa na meno;

(g) Matibabu ya macho, masikio, pua, ngozi na koo;

(h) Huduma za mazoezi ya viungo;

(i) Huduma za usafishaji figo;

(j) Huduma za saratani;

(k) Huduma za uzazi;

(l) Huduma za mama na mtoto;

(m) Huduma za matibabu ya kibingwa;

(n) Huduma za magonjwa ya akili;

(o) Huduma za dharura;

(p) Huduma za wagonjwa mahututi;

(q) Huduma za vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu; na

(r) Huduma za marekebisho kwa watu wenye ulemavu.

2. Huduma za matibabu zinazotolewa chini ya Sheria hii hazitajumuisha gharama za huduma zilizoainishwa hapa chini:

(a) vipodozi na upasuaji wa mapambo;

(b) utoaji mimba usiohalali; na

(c) dawa zisizoidhinishwa na daktari na vifaa tiba.

3. Bila ya kuathiri masharti ya kipengele cha 1 cha Jadweli hili, mwanachama yeyote atakayehitaji kufanya vipimo vya CT SCAN, MRI na vipimo vyengine vinavyofanana au matibabu mengine yenye gharama za juu kama vile saratani na usafishaji wa figo itahitajika kwanza kupata ruhusa kutoka katika Mfuko kabla uchunguzi huo haujafanywa isipokuwa katika hali ya dharura.

UMEPITISHWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 28 Februari, 2023.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***